# Tamko la HakiElimu Kuhusu Upangaji wa Bajeti ya Elimumsingi Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Utangulizi**

Bajeti ya Sekta ya Elimu ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa mipango ya serikali ya utoaji huduma ya elimu nchini. Hata hivyo ili mpango wa bajeti uweze kuwa na ufanisi, ni muhimu uandaaji wake uzingatie ushiriki na michango ya wadau mbalimbali juu ya mahitaji na vipaumbele vya sekta hiyo. HakiElimu, tukitambua kuwa sisi ni sehemu ya wadau hao muhimu, tumefanya uchambuzi wa mahitaji muhimu ya kibajeti ambayo yanapaswa kupewa uzito katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Uchambuzi huu, umezingatia ukweli kwamba zipo juhudi kubwa kwa upande wa serikali za upanuzi na uboreshaji wa elimumsingi zinazoendelea zikichagizwa na utekelezaji wa "elimumsingi bila malipo". Katika kutekeleza agizo hili la kisera, serikali imeendelea kutumia sehemu kubwa ya bajeti yake (zaidi ya 60% ya bajeti nzima ya sekta) kuhudumia elimumsingi. Mathalani Mwaka 2016/17 serikali iliidhinisha shilingi bilioni 4,768 kama bajeti ya sekta nzima ya elimu lakini shilingi bilioni 3,020 (sawa na 63.3%) zilitengwa kwa ajili ya kuhudumia elimumsingi (BEST, 2016). Kwa sababu hii, ushiriki wa wadau na wananchi katika kuamua vipaumbele vya fedha hii kubwa ni muhimu sana ili kuleta matokeo tarajiwa.

Hivyo wakati bajeti ya serikali kupitia wizara zake inawasilishwa na kujadiliwa Bungeni ili kupitishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za huduma na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018, HakiElimu inatoa mapendekezo ya vipaumbele na maeneo ya kuzingatiwa katika bajeti ya sekta ya elimu (hasa elimumsingi) katika mwaka wa fedha 2017/2018.

**1. Eneo la Bajeti ya uboreshaji na ujenzi wa miundombinu shuleni**

Ni muhimu kwa serikali kuzingatia ongezeko kubwa la udahili wa wanafunzi hasa katika shule zetu za msingi kutokana na utekelezaji wa elimu bila malipo. Kwa mujibu wa takwimu za elimu (BEST, 2016) Udahili kwa madarasa ya awali umeongezeka kwa takribani asilimia 46 sawa na ongezeko la wanafunzi 492,947 huku ule wa shule za msingi ukiongezeka kwa asilimia 41sawa na wanafunzi 552,289 kwa kulinganisha na udahili wa Mwaka 2015.

Hili ni ongezeka la takribani watoto wapya 1,000,000 shuleni. Kwa wastani wa wanafunzi 45 kila darasa, watoto hawa watahitaji takribani vyumba vipya 22,222 vya madarasa ambavyo gharama

zake ni takribani shilingi bilioni 267 kwa gharama ya shilingi milioni 12[1] kwa darasa. Ikumbukwe kuwa kabla ya ongezeko hili la wanafunzi shule za umma zilikuwa na upungufu wa miundombinu ya madarasa 95,945 (BEST, 2016); wastani wa uwiano kati ya mwanafunzi kwa darasa shule za msingi za umma ni 1:77 (BEST 2016). Upungufu wa vyumba 95,945 gharama yake ni takribani bilioni 1,151. Hivyo tukijumulisha na ongezeko la wanafunzi baada ya kuanza utekelezaji wa elimu bila malipo, serikali itahitaji kutenga kiasi cha takribani bilioni 1,418 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mapya kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018.

Bajeti ni lazima izingatie pia uhaba wa miundombinu ya vyoo na vifaa vya kufundishia ambao umeendelea kukua. Mathalani, uwiano wa mwanafunzi wa kike shule za msingi kwa tundu la choo ni wanafunzi 57 kwa tundu moja la choo (1:57) badala ya wanafunzi 20 (1:20) kwa tundu la choo; wakati kwa wanafunzi wa kiume, watoto 56 wanalazimika kuchangia tundu moja la choo badala ya wanafunzi 25 tu.. Hii ina maana kuwa upungufu wa matundu ya choo kwa watoto wa kiume shule za msingi ni takribani asilimia 56 ya mahitaji na kwa watoto wa kike upungufu ni 62.

Aidha elimu msingi inaendelea kukabiliwa na uhaba wa nyumba za walimu zipatazo 186,008 (upungufu wa asilimia 81.1); majengo ya utawala yapatayo 10,943 (sawa na upungufu wa 83.4%); vyumba vya maktaba vipatavyo 15,342 (sawa na upungufu wa 88%) na ukosefu wa vyumba vya huduma ya kwanza kwa asilimia 93.9% (sawa na mahitaji ya vyumba 16,290).

Takwimu hizi zinaonesha upungufu mkubwa wa miundombinu unaohitaji juhudi za makusudi za kibajeti ili kuikwamua elimumsingi katika hali hii. Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti ya Benki ya Dunia (SDI Report 2016, kwa wastani ni asilimia 41 ya shule za msingi na sekondari ndizo zilizo na miundombinu inayokidhi mahitaji ya shule. Ni rai yetu kuwa bajeti ya sekta ya elimu kwa mwaka wa fedha 2017/18 itazingatia mahitaji haya na kutenga fedha za kutosha hasa katika bajeti ya maendeleo ili kuweza kusaidia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu kwa elimumsingi.

### 2. Uhaba wa walimu shuleni

Pamoja na kuwa wastani wa uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi kwa shule za msingi umeimarika hadi kufikia 1:43 (mwalimu mmoja anafundisha watoto 43), lakini hali ni mbaya kwa shule moja moja na kwa mahudhurio ya walimu hawa darasani. Ripoti ya SDI 2016 ya Benki ya dunia inabainisha kuwa, pamoja na kuwa walimu walioajiriwa ni wengi lakini mahudhurio yao darasani yanatia shaka. Kwa mujibu wa ripoti hii ni asilimia 49 tu ya walimu walioajiriwa ndio

[1] Gharama za makadirio ya Ujenzi wa darasa moja kwa mujibu wa BEST, 2015

wanaingia darasani na kufundisha kama inavyotakiwa huku asilimia 32 wanafika shuleni lakini hawafundishi na asilimia 14 ya walimu walioajiriwa hawafiki kabisa shuleni.

Takwimu za Chama cha Walimu nchini (CWT), zinaonesha kuwa shule za msingi peke yake zina upungufu wa takribani walimu 100,000 kwa kuangalia kigezo cha majukumu waliyonayo (Workload). Shule za sekondari zina upungufu wa walimu 50,000 wakiwemo walimu 30,000 wa masomo ya sayansi na walimu 20,000 wa masomo ya sanaa. Takwimu za serikali (BEST, 2016) zinaonesha kuwa kuna uhaba wa walimu wa masomo ya hesabu wapatao 7,291, walimu 5,181 wa somo la baiolojia, walimu 5,373 wa somo la kemia na walimu 6,873 wa somo la fizikia.

Shule za umma zinakabiliwa pia na upungufu wa watumishi wataalamu wa maabara 4,000. Takribani 90% ya shule zote za sekondari za kata ambazo ni zaidi ya 3,500 hazina wataalamu wa maabara, hivyo kuongeza mzigo kwa walimu wa kawaida kushughulika na uandaaji wa majaribio na utunzaji wa vifaa vya maabara. Kuwepo kwa wataalamu hawa si tu kutapunguza mzigo kwa walimu lakini pia kutaongeza ufanisi katika kuandaa wanasayansi ambao ni nguzo kubwa katika kusaidia mapinduzi ya viwanda kama kusudio la serikali lilivyo.

Kwa sababu hizi, HakiElimu tunaishauri Serikali na Bunge kuihuisha bajeti ili kuajiri walimu na wataalamu wa maabara wanaotakiwa ili kufidia pengo hili pamoja na kutenga bajeti inayostahili kuwamotisha walimu ili watulie katika vituo vyao wakifanya kazi.

### 3. Bajeti ya ulipaji madeni na malimbikizo ya walimu

Kwa mujibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT); takribani walimu wastaafu 1,097 wanaidai serikali kiasi cha shilingi bilioni 138, ikiwa ni madai ya mafao yao na pensheni kutoka mfuko wa hifadhi ya jamii wa PSPF. Hili ni deni la serikali kwa walimu hawa ambalo PSPF imeshindwa kuwalipa wastaafu hawa kwa kuwa serikali haijapeleka fedha za wastaafu hao katika mfuko huu. Hivyo tunaishauri serikali kupanga bajeti ya kulipa mafao haya PSPF ili hatimaye walimu hawa wastaafu waweze kulipwa stahili zao.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa CWT Bw. Ezekiel Oluoch, walimu takribani 80,000 waliopandishwa madaraja kati ya Februari na Machi 2016 bado wanaidai serikali zaidi ya bilioni 200 ikiwa ni malipo ya malimbikizo ya ongezeko la mshahara kutokana na kupandishwa daraja. Walimu pia hadi kufikia Disemba 2015 walikuwa wanadai malipo yasiyotokana na mshahara yafikiayo takribani bilioni 9 baada ya uhakiki ambayo bado hayajalipwa mpaka sasa.

Hata hivyo takribani shilingi bilioni 11 za malipo yasiyokuwa ya mishahara yalikataliwa na serikali baada ya uhakiki kutokana na sababu mbalimbali. Ni rai yetu kuwa walimu ambao madai yao yalikataliwa wapewe taarifa kwa maandishi wakielezewa sababu za kukataliwa huko na wapewe nafasi ya kukata rufaa ikiwa wataona inafaa. Ni muhimu hatua hii kufanyika kwa kuwa madai mengine halali yalikataliwa kwa vigezo vya kukosea taratibu tu za uombaji ambazo hazibatilishi deni halisi.

Kwa mujibu wa CWT madai ya walimu yasiyokuwa ya mishahara yanatarajiwa kuongezeka kwa shilingi bilioni 10 zaidi, yakijumlishwa na malimbikizo ya Januari hadi Desemba 2016 uhakiki utakapokamilika. Ushauri wetu kwa serikali ni kuwa uhakiki huu uharakishwe na ukamilike mapema ili kuruhusu wizara na idara kupanga fedha za kulipa madeni haya katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18.

Tunaishauri serikali pia kutenga takribani shilingi bilioni 90 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18 kwa ajili ya kuwalipa walimu takribani 150,000 wanaotarajiwa kuchukua likizo za malipo kwa wastani wa shilingi 600,000 kila mmoja katika mwaka ujao wa fedha. Lakini ili kuepusha adha ya walimu kwenda likizo bila kupata malipo na kusababisha kuongezeka kwa madeni ya walimu, tunaishauri serikali kukubali pendekezo la CWT la kuanzisha mshahara wa 13 kwa walimu wote ambao utafidia usumbufu wa fedha za likizo kila zinapohitajika na ikiwezekana utaratibu wa mshahara huu uanze katika bajeti ijayo ya mwaka wa fedha 2017/18.

## 4. Utekelezaji wa bajeti ya Maendeleo ya Elimu.

Kwa mujibu wa Waziri wa Fedha, Ndugu Philip Mpango kumekuwa na utekelezaji wa bajeti pungufu ya maendeleo kwa Mwaka 2016/17. Hadi kufikia Mwezi Machi 2017 serikali ilikuwa imetoa asilimia 34% tu ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ya Bajeti ya Taifa, jambo ambalo limeathiri pia bajeti ya maendeleo ya sekta ya elimu. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya Tsh bilioni 897.6 ziliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo. Katika mgawanyo wa fedha hizi, Tsh bilioni 427 (asilimia 48) ziliidhinishwa kwa ajili ya kugharamia mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na Tsh bilioni 470 (asilimia 52) ziliidhinishwa kwa ajili ya kugharamia miradi halisi ya maendeleo ya sekta ya elimu inayotekelezwa na Wizara kama ujenzi wa miundombinu ya shule na vyuo.

**Mgawo wa fedha za Maendeleo za Wizara ya Elimu 2016/17 (Tsh.Bilioni)**




*(Chanzo; Randama ya Bajeti ya Fungu namba 46, 2017/18)*

Hatari iliyopo katika utekelezaji wa bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Elimu ni kuwa sehemu kubwa ya fedha zilizotolewa mpaka mwezi Machi 2017 zilikuwa ni kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na sehemu kidogo kwa ajili ya miradi halisi ya maendeleo kama ujenzi wa miundombinu. Mathalani, kwa mujibu wa randama ya bajeti ya Wizara ya Elimu fungu namba 46 ya mwaka 2017/18, jumla ya shilingi bilioni 344 sawa na asilimia 80 ya fedha zote za mikopo ya elimu ya juu shilingi bilioni 427 zilikuwa zimeshatolewa kwa matumizi hadi kufikia Machi 2017. Wakati huo huo ni shilingi bilioni 156.4 pekee ambazo ni sawa na asilimia 30 tu ya fedha za miradi halisi ya maendeleo zilizoidhinishwa ambazo ni shilingi bilioni 470 zilikuwa zimetolewa hadi Machi 2017.







*(Chanzo; Randama ya Bajeti ya wizara, Fungu na 46 2017/18)*

Kwa hiyo, hii ni sawa na kusema kuwa kati ya shilingi bilioni 500.4 zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wizara ya Elimu, sehemu kubwa ya fedha hizi, ambazo ni shilingi bilioni 344.3 (takribani 70%) zimetolewa kwa ajili ya kugharamia utoaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Hii ina maana kuwa ni shilingi bilioni 156.1 pekee sawa na 30% ya fedha zilizotolewa ndiyo inayokwenda kwenye miradi halisi ya maendeleo ya Wizara ya Elimu. Hivyo kati ya shilingi bilioni 897.6 zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya wizara ya elimu, ni shilingi bilioni 156.1, sawa na asilimia 17% tu ya fedha ya maendeleo ndiyo iliyotolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi halisi ya maendeleo ya wizara (Ukiondoa fedha iliyotolewa kama mikopo ya elimu ya juu) hadi kufikia Machi 2017.







*(Chanzo; Randama ya Bajeti ya wizara, Fungu na 46 2017/18)*

Ni wazi kuwa mwenendo huu wa utekelezaji bajeti ya maendeleo si mzuri na hauwezi kutatua changamoto za uwekezaji katika elimu na taifa letu. HakiElimu tunaishauri Serikali na Bunge kuzingatia mwenendo huu wa utoaji fedha za mandeleo wakati wa upangaji wa bajeti ya sekta ya elimu kwa mwaka wa fedha 2017/18. Hali ya upelekaji wa bajeti pungufu zaidi ya iliyoidhinishwa si tu inarudisha nyuma utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika elimu lakini pia unaleta mkanganyiko katika upangaji na ugawanyaji wa rasilimali, na wakati mwingine inapoteza maana halisi ya upangaji wa bajeti. Tunaitaka serikali kuzingatia upangaji wa bajeti inayotekelezeka.

**Utegemezi wa bajeti kwa wahisani;** Serikali na Bunge pia wazingatie mwenendo usioridhisha wa utoaji fedha wa wahisani na washirika wa maendeleo ili kuweza kufanya upangaji wenye uhalisia. Katika bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Elimu iliyoidhinishwa Mwaka wa fedha

2016/17, takribani bilioni 277 sawa na asilimia 31% ilitarajiwa kukusanywa kutoka kwa wahisani na washirika wa maendeleo. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Machi 2017, wahisani walikuwa wametoa kiasi cha shilingi bilioni 132 tu, (sawa na asilimia 47.6%). Kwa sababu hii ni muhimu serikali kuendelea kuimarisha vyanzo vyake vya mapato vya ndani na tunaishauri kutumia fedha za ndani kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu ili kuepusha adha hii ya utekelezaji wa bajeti pungufu kila mwaka.

## 5. Bajeti ya Udhibiti Ubora wa Shule

Mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilipangiwa kutumia shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya shughuli za udhibiti ubora. Katika kipindi cha utekelezaji cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Wizara ya Elimu imepokea jumla ya shilingi milioni 382 sawa na 16% tu ya fedha iliyoidhinishwa. Hii inatoa tafsiri kuwa shughuli nyingi za udhibiti ubora hazikuweza kufanyika katika mwaka wa fedha 2016/2017. Lazima tutambue kuwa udhibiti ubora wa shule ni muhimu sana kwa wizara kwani ndio huisaidia kuweza kufanya ukaguzi wa shule na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa walimu ili waweze kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji na hatimaye kuboresha elimu yetu.

Miaka ya 2014 na 2015 hali ya ukaguzi imekuwa si nzuri kwa idara hii muhimu kwa sababu ya changamoto za fedha. Kwa mujibu wa takwimu, (BEST 2015) ni wastani wa 20% tu ya idadi ya shule za msingi na sekondari hukaguliwa kwa mwaka. Kwa kuangalia kiwango cha asilimia 16 ya fedha zilizotolewa ni wazi kuwa asilimia kidogo zaidi ya shule zitafanyiwa ukaguzi katika kipindi cha 2016/17. HakiElimu tunalishauri Bunge na Serikali kuzingatia mapungufu haya ya kibajeti wakati wakipanga bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18 ili kuona wapi kwa kurekebisha au kutilia mkazo.

## 6. Bajeti ya utekelezaji wa miradi ya Elimu:

Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kuanzia Julai 2016 hadi Machi 2017 imeainisha mapungufu makubwa katika utekelezaji wa bajeti ya miradi mtambuka ya Elimu iliyopangwa kutekelezwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2016/17. Miradi hiyo ambayo utekelezaji wake umeathirika kutokana na kutolewa kwa bajeti pungufu ya maendeleo ni pamoja na Programu za Maji na Usafi shuleni (WASH), Programu za Uimarishaji wa mafunzo ya KKK chini ya LANES, bajeti ya Ukaguzi na kuimarisha ubora wa Shule. Ufafanuzi wa aina ya mradi, kiwango kilichopangwa na kilichotolewa hadi kufikia Machi 2017 unatolewa katika jedwali hili chini;-

| Na. ya Mradi | Jina la Mradi | Bajeti iliyopangwa | Fedha iliyotolewa hadi Machi 2017 | % ya Mapokezi |
|---|---|---|---|---|
| PT4321 | Kuimarisha Mafunzo ya KKK chini ya LANES | Tsh bil 108 | Tsh bil 29.2 | 27% |
| PG3280 | Mradi wa Maji na Usafi Shuleni (SWASH) | Tsh mil 607.3 | Tsh mil 180 | 29% |
| PT6235 | Kuimarisha Udhibiti Ubora wa Shule | Tsh bil 8.7 | 0 | 0% |
| PT4320 | Kuimarisha Taasisi ya Elimu | Tsh bil 42.7 | 0 | 0% |
| PT4371 | Ukarabati wa vyuo vya ualimu | Tsh bil 23 | 0 | 0% |
| PT4370 | Mpango wa Elimu kwa walioikosa wa "Ndiyo Naweza" | Tsh bil 2.3 | 0 | 0% |
| T4306 | Ukarabati wa ADEM | Tsh bil 1 | 0 | 0% |
| | | | | |
| **TOTAL** | | **Tsh bil 186.3** | **29.38** | **16%** |

*(Chanzo; Randama ya Bajeti ya wizara, Fungu na 46 2017/18)*

Kwa hiyo ni sawa na kusema kati ya takribani shilingi bilioni 186 zilizotengwa kwa ajili ya miradi mikuu ya maendeleo kwa Wizara ya Elimu ni shilingi bilioni 29 tu, sawa na asilimia 16 pekee ya fedha zilizoidhinishwa, ndizo zilitolewa hadi kufikia Machi 2017. Kwa mwenendo huu miradi hii haitakuwa imefikia walau asilimia 30 ya utekelezaji hadi mwisho wa mwaka wa fedha wa 2016/2017. Hali hii ni hatari kwa shughuli za maendeleo ya sekta ya elimu na inaturudisha nyuma hatua nyingi zaidi.




Kwa tafsiri hii, ni dhahiri kuwa bado kunahitajika juhudi kubwa ili kuweza kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia. Ni rai yetu kwa wabunge hasa kupitia kwa makini utekelezaji wa miradi hii ili kuweza kuishauri vizuri serikali katika mipango yake.

## 7. Bajeti ya fedha ya ruzuku shuleni

Maamuzi ya serikali ya kutekeleza agizo la kisera la utoaji elimumsingi bila malipo kunatoa wajibu kwa serikali kuendelea kuziwezesha shule za msingi kwa ruzuku ya Tsh. 10,000 kwa kila mwanafunzi na ruzuku ya Tsh. 25,000 kwa sekondari pamoja na kufidia ada ya Tsh. 20,000 kwa shule za kutwa na Tsh. 40,000 kwa shule za bweni za sekondari na kugharamia uwekezaji kama ujenzi wa miundombinu na vifaa vya kufundishia.

Katika waraka Elimu namba 3 wa mwaka 2016, serikali ilibainisha kupeleka shuleni asilimia 60 ya Tsh 10,000 ambayo ni sawa na Tsh 6,000 na asilimia inayobaki ambayo ni Tsh 4,000 kwa kila mwanafunzi kubaki TAMISEMI kwa ajili ya ununuzi wa vitabu ambavyo vingepelekwa moja kwa moja shuleni. Utafiti uliofanywa na Shirika la HakiElimu mwishoni mwa Mwaka 2016 juu ya utekelezaji wa elimu bila malipo unaonesha kuwa, shule za msingi zilipokea wastani wa shilingi 500 kwa mwezi kwa kila mtoto ambayo ni sawa na Tsh. 6,000/= kwa mwaka kwa kila mtoto.

Hata hivyo, takribani 94.6% ya wakuu wa shule waliohojiwa walithibitisha kuwa kiwango cha ruzuku cha Tsh. 6,000 kilichotolewa kwa mwaka 2016 kwa mwaka kwa kila mtoto hakitoshi kugharamia mahitaji yote ya shughuli za utawala, gharama za mitihani na ukarabati wa miundombinu na manunuzi madogo madogo. Walimu hao walisema, pamoja na kuwa fedha inafika shuleni; lakini kiwango hicho kimekuwa hakitoshi kukidhi mahitaji yaliyokusudiwa hasa katika kipindi hiki ambacho ushiriki wa wazazi umepungua kwa kiwango kikubwa. Kwa mujibu wa walimu hao waliohojiwa viwango hivyo si tu kuwa ni vya chini lakini pia vimepitwa na wakati na vinahitaji kufanyiwa marekebisho ili viendane na mahitaji.

Ni dhahiri kuwa kiwango cha shilingi 10,000 kwa shule za msingi na 25,000 kwa sekondari ambavyo vilipangwa mwaka 2001 vimeshuka thamani. Mathalani, ruzuku kwa shule za msingi katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi wa kwanza ilipangwa dola 10 kwa kila mwanafunzi ambapo kipindi hicho dola 1 ilikuwa shilingi 1,000 na hivyo ruzuku ikathaminishwa kama shilingi 10,000. Hivi sasa dola imepanda na thamani ya shilingi imezidi kushuka ambapo dola 1 ni shilingi 2,200. Hivyo kimsingi ruzuku kwa shule za msingi ilipaswa iwe angalau shilingi 22,000 na shilingi 50,000 kwa sekondari.

Kwa sababu hii, ili serikali iweze kugharamia utoaji wa elimu bure ni lazima ifanye marekebisho ya viwango vya ruzuku kwa kuzingatia kushuka kwa thamani ya shilingi ikilinganishwa na nguvu ya manununuzi iliyokuwa nayo miaka ya 2001 wakati viwango hivi vinapangwa. Hivyo

HakiElimu tunaishauri serikali na bunge, kupanga na kuidhinisha walau ruzuku ya shilingi 22,000 kwa kila mwanafunzi wa msingi na walau 50,000 kwa kila mwanafunzi wa sekondari; na kwa sababu hiyo katika mwaka wa fedha 2017/18 serikali itatakiwa kutenga takribani bilioni 306.5 kama fedha za ruzuku na fidia ya ada kwa mwaka wa fedha ujao. Kiwango hiki kinafafanuliwa vizuri katika jedwali hapa chini:-

**Jedwali Namba 1: Makadirio ya Ruzuku na Fidia ya ada kwa Bajeti ya 2017/2017**

| | Kiasi (Tsh) | Idadi ya Wanafunzi | Jumla |
|---|---|---|---|
| Elimu ya awali | 20,000 | 1,562,770 | Bil 32 |
| Msingi | 20,000 | 8,987,031 | Bil 180 |
| Sekondari | 40,000 | 1,575,254 | Bil 63 |
| Ada Sekondari | 20,000 | 1,575,254 | Bil 31.5 |
| **Jumla ya Ruzuku Msingi na Sekondari** | | | **Bil 306.5** |

**Hitimisho**

HakiElimu tunatambua majukumu makubwa ambayo serikali inayo katika kutoa huduma za jamii kwa ujumla. Hata hivyo elimumsingi ndiyo mlango wa upatikanaji huduma nyingine. Kama watoto wetu watajengwa vizuri kitaaluma, wataweza kuja na mbinu za kutatua changamoto nyingine katika sekta nyingine ikiwamo ya ukuzaji viwanda na uchumi.

Serikali izingatie maeneo yaliyotajwa hapo juu wakati wa upangaji wa bajeti ya sekta ya elimu wakizingatia pia kuwa mipango hiyo inapaswa kuwa jumuishi. Mathalani, upande wa miundombinu bado shule nyingi hazijaweka mazingira rafiki kwa ajili ya watoto wenye ulemavu na mahitaji maalumu.

Bajeti pia iangalie uwezekano wa kuanzisha na kugharamia bajeti ya utoaji uji au mlo shuleni hasa kwa watoto wa elimu ya awali na madarasa ya chini kwa shule za msingi ili kuwawezesha kuhimili muda na wawe na umakini wanapokuwa shuleni na darasani.

Bajeti pia itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kuendelea kuimarisha udhibiti ubora shuleni ili kuinua taaluma. Takwimu zinaonesha kuwa uwezo serikali kufanya ukaguzi washule bado uko chini ya 50% kwa mwaka kutokana na ufinyu wa bajeti.



**John Kalage**

**Mkurugenzi Mtendaji-HakiElimu**